ELIMU YA KUJITEGEMEA

Hotuba hii ilitolewa Machi 1967 na Rais wa Kwanza
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Julius K. Nyerere.

"Ni wazi wakati umefika sasa tufikirie sana juu ya swali hili: 'Mpango wa Elimu Tanzania umewekwa kwa sababu gani-shabaha yake ni nini?"
Julius K. Nyrere 1967

Dar es Salaam
Machi 1967

ELIMU YA KUJITEGEMEA

Tangu siku nyingi kabla ya uhuru watu wa nchi hii, chini ya uongozi wa TANU, wamekuwa wakidai elimu zaidi kwa watoto wao. Lakini bado hatujakaa na kufikiri kwa nini tunataka elimu: ina shabaha gani. Kwa hiyo, ingawaje kwa siku nyingi mafunzo yanayotolewa katika shule yametolewa makosa, lakini mpaka sasa hatujaitoa makosa misingi yenyewe ya elimu tuliyoirithi wakati tulipopata uhuru wetu. Hatujafanya hivyo kwa sababu kwa kweli hatujafikiria bado habari ya mipango ya elimu, isipokuwa katika kupata walimu, mainjinia, mabwana shauri, n.k. Kila mtu binafsi, na hata sote kwa pamoja tumefikiria elimu kama mafunzo ya kazi ya kujipatia mishahara mikubwa katika kazi za kisasa.

Sasa inafaa tufikirie tena kama ni haki kwa nchi maskini kama yetu kutumia zaidi ya 20 kwa mia ya fedha za Serikali kwa ajili ya kuwapatia elimu watoto na vijana wetu, na tuanze kufikiri elimu hiyo itatufaidia nini. Maana katika hali yetu haiwezekani kutenga Shs.147,330,000 kila mwaka kuwasomeshea baadhi tu ya watoto wetu, (wakati watoto wengine wanakosa) ila tu kama matokeo ya elimu hiyo yatalifaidia Taifa tunalotaka kulijenga.

Mipango ya elimu katika nchi mbali mbali duniani siku zote inahitilafiana, katika muundo wake na elimu itolewayo. Mipango hiyo huhitilafiana kwa sababu nchi zenyewe zinazotoa elimu huhitilafiana, na kwa sababu elimu yoyote, iwe ya darasani, au si ya darasani ina shabaha yake. Shabaha yenyewe ni kurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine maarifa na mila za taifa, na kuwaandaa vijana wawe tayari kuchukua nafasi zao katika kulitumikia na kuliendeleza taifa.

Hivi ndivyo ilivyo katika nchi zote: katika nchi za Kikabaila za Magharibi, nchi za Kikomunisti za Mashariki na hata zilivyokuwa nchi za Kiafrika kabla ya Ukoloni.

Maana si kweli kusema kwamba kabla ya ukoloni Waafrika hawakuwa na elimu, eti kwa sababu tu hawakuwa na shule, na kwamba makabila machache yalitoa mafunzo kwa muda mfupi tu kambini. Hawa walijifunza kwa kuishi na kutenda. Nyumbani kwao, au shambani kwao, walijifunza ufundi wa kazi zilizopaswa kufanywa, pamoja na tabia wanayopaswa kuwa nayo watu wa jamaa ile. Walijifunza aina za majani na mizizi ya miti ya porini na kazi zake; walijifunza jinsi ya kushughulikia mavuno, au jinsi ya kuangalia mifugo, kwa kuzifanya kazi hizo pamoja na wale walio wakubwa kuliko wao. Walijifunza historia ya kabila lao, na uhusiano baina ya kabila lao na makabila mengine, na uhusiano baina ya kabila lao na mizimu, kwa kusikiliza tu hadithi zilizokuwa zikitolewa na wazee.

Kwa njia hizi, na kwa desturi za kushirikiana walizofunzwa vijana, mila za nchi ziliendelezwa. Kwa hiyo elimu waliyopata haikuwa ya kujifunza darasani; kila mtu mzima alikuwa mwalimu kwa njia yake. Lakini kukosa madarasa maana yake si kwamba hakukuwako elimu, wala hakukupunguza umuhimu wa elimu katika Taifa. Na kwa kweli inawezekana elimu aliyokuwa akiipata kijana enzi zile ijapo si ya darasani, ilikuwa elimu inayomfaa kuishi katika jamaa yake.

Huko Ulaya elimu ya darasani imekuja siku nyingi. Lakini tukifikiria jinsi ilivyofikia hali hiyo tutaweza kuona kwamba shabaha yake ni kama ile ile ya mtindo wa Kiafrika wa kiasili. Yaani shabaha ya elimu ya darasani huko Ulaya ilikuwa kuimarisha mila zilizokuwa zikitumika katika nchi, na kuwaandaa watoto na vijana kutimiza wajibu wao katika nchi hiyo. Na hivyo hivyo ndivyo ilivyo katika nchi za Kikomunisti siku hizi. Mafunzo yanayotolewa ni tofauti na yale yanayotolewa katika nchi za magharibi, lakini shabaha ni moja: kuwaandaa vijana kuishi katika Taifa hilo, na kuendeleza busara, ujuzi na mila za taifa katika kizazi kijacho. Mahali popote ambapo elimu inashindwa kutimiza shabaha hizo, basi maendeleo ya nchi hiyo yatalegalega, la sivyo kutatokea malalamiko watu watakapogundua kwamba elimu yao imewaandaa kuishi maisha ambayo kwa kweli hayapo.

Elimu ya Kikoloni Tanzania na Jinsi ambavyo Taifa Letu Lilivyoirithi

Elimu iliyokuwa ikitolewa na serikali ya mkoloni katika nchi zile mbili, Unguja na Tanganyika, ambazo sasa ni Tanzania, ilikuwa na shabaha tofauti. Haikupangwa ili kuwaandaa vijana kutumikia taifa lao; badala yake ilipangwa kwa kutimiza haja za kuingiza desturi za kikoloni. Kwa hiyo haja ya elimu katika nchi hizi ilitokana na haja ya kuwa na makarani na maofisa wa vyeo vya chini, na vile vile vikundi mbalimbali vya dini vilitoa mafunzo ya kusoma na kuandika, na elimu nyingine, kama njia ya kueneza imani yao.

Shabaha ya kuutaja ukweli huu siyo kukashifu wale wengi waliofanya kazi ngumu sana, mara nyingi kwa shida kubwa, katika kufundisha na kuweka mipango ya elimu. Wala sisemi kwamba yote waliyoyafundisha katika mashule yalikuwa ya kupotosha na yasiyofaa. Ninavyosema ni kwamba elimu iliyotolewa na mkoloni katika Tanzania ilikuwa ya mtindo wa Kiingereza, lakini mkazo wake wa fikara za ubwana na kufanya kazi za ofisini ulikuwa mkubwa zaidi hata kuliko ilivyokuwa kule Uingereza. Kadhalika elimu hiyo ilikuwa imepangwa kwa mtindo wa kikabaila. Ilitilia mkazo fikara za kila mtu kuishi peke yake, badala ya mawazo ya kushirikiana. Iliwafanya watu wafikiri kwamba dalili ya heshima ya mtu katika taifa ni kujilimbikizia mali nyingi.

Ndiyo kusema kwamba elimu ya kikoloni ilileta fikara za mtu kuwa bwana na wengine watwana, na kwa kweli iliwafanya wanyonge wakandamizwe na wenye nguvu, hasa matajiri. Kwa hiyo elimu ya kikoloni katika nchi hii haikuwa ya kuendeleza ujuzi na mila za Watanzania kutoka kizazi kimoja hadi kingine; ilikuwa na juhudi hasa ya kubadili mawazo hayo na badala yake kupanda mila na ujuzi kutoka nchi nyingine.

Na hivyo ilikuwa sehemu ya juhudi ya kuleta mapinduzi ya mawazo katika nchi; kuyageuza yawe ya watu wa kikoloni wanaokubali hali hiyo, mawazo yatakayokuwa ya msaada kwa Serikali inayotawala. Pengine hawakufaulu katika shabaha hiyo, lakini hiyo siyo kusema kwamba wameshindwa kugeuza fikara, tabia ya wale waliopitia shule zao. Wala kushindwa huko maana yake siyo kusema kwamba elimu iliyotolewa enzi ya ukoloni ilikuwa na shabaha ya kuwalea watu wanaoamini usawa wa binadamu.

Kwa kweli nchi huru ya Tanzania ilirithi mtindo wa elimu ambayo kwa njia nyingi ilikuwa haitoshi wala haifai kwa haja za nchi hii. Lakini kulikodhihirika mapema zaidi ni kutokutosha kwa elimu. Elimu iliyotolewa ilikuwa kidogo mno. Mwezi Desemba 1961, watu wenye elimu ya kutosha walikuwa wachache mno wala wasingetosha kuendesha Serikali ya siku zile, wacha kazi zingine za mipango ya maendeleo zilizokuwa muhimu zaidi. Wala idadi ya watoto waliokuwa shuleni mwaka 1961 haikuwa kubwa ya kutoa matumaini kwamba hali hii ingeweza kurekebishwa haraka. Juu ya hivyo, elimu iligawiwa kwa mataifa, ambapo msingi wa madai yetu yote ya uhuru ulikuwa ni kulaani kabisa ubaguzi wa rangi.

Vitendo Baada ya Uhuru

Makosa matatu makubwa ya elimu tuliyoirithi tumekwisha yataja. Kwanza, ubaguzi wa rangi katika kugawa elimu ulifutwa. Mara tu baada ya uhuru ulianzishwa mpango wa kuunganisha kabisa shule za mataifa yote, na ubaguzi kutokana na dini pia ukakomeshwa. Sasa mtoto wa Tanzania anaweza kusoma katika shule yoyote ya Serikali, au shule yoyote inayosaidiwa na Serikali katika nchi hii, bila ya kujali rangi au dini yake, na bila hofu kwamba gharama ya elimu yake ni kufundishwa dini nyingine.

Pili, nafasi za masomo zimeongezwa sana, hasa katika shule za Sekondari na za Vyuo vya juu. Katika mwaka 1961 walikuwako watoto 490,000 waliokwenda katika shule za msingi katika Tanganyika, wengi wao wakafika darasa la 4 tu. Katika mwaka 1967 watoto 825,000 wanakwenda shule hizo, na wanaomaliza

darasa la saba wanazidi kuongezeka. Vile vile, mwaka 1961 kulikuwako watoto 11,832 katika shule za Sekondari, na 176 tu ndio waliokuwa darasa la 14. Mwaka huu, tuna wanafunzi 25,000 katika shule za Sekondari, na 830 wako darasa la 14. Kwa kweli haya ni mafanikio ambayo nchi yetu changa inaweza kujivunia. Inafaa tujikumbushe kwamba matatizo ya sasa (hasa shida zinazosemekana za watoto wanaomaliza darasa la saba) ni matatizo yaliyoletwa na mafanikio haya.

Jambo la tatu tulilolifanya ni kuifanya elimu inayotolewa katika shule zetu zote iwe ya ki-Tanzania zaidi katika muundo wake. Watoto wetu sasa hawajifunzi historia ya Kiingereza na ya Ulaya peke yake. Kwa haraka zaidi kuliko tulivyodhania imewezekana Chuo chetu Kikuu na Vyuo vingine kutoa sasa vitabu vya historia za kiafrika na kuwapa walimu wavitumie. Watoto wetu wamerudia kufundishwa nyimbo na ngoma zetu za Taifa. Lugha yetu ya Taifa inatiliwa mkazo unaostahili katika masomo. Kadhalika mafunzo ya Uraia yanaanza kuwapa nafasi wanafunzi wa shule za Sekondari kuelewa muundo na shabaha za Taifa letu changa. Kwa njia hizi, na njia zingine, yameletwa mabadiliko kufanya mtindo wetu wa elimu ufanane na haja zetu. Kwa wakati huu ambapo watu wanadadisi kazi zinazofanywa, (na haki yao waulize), inafaa tushukuru kazi inayofanywa na walimu wetu, na wale wanaoangalia kazi yao katika Wizara, katika Chuo cha Ualimu, katika Chuo Kikuu na Halmashauri za Wilaya.

Lakini yote haya niliyoyataja ni mabadiliko kidogo tu juu ya mtindo ule tuliourithi. Matunda yake hayajaonekana bado; inachukua miaka mingi mpaka mabadiliko ya mtindo wa elimu yazae matunda. Ila mambo yaliyotokea mwaka 1966 yanadhihirisha kwamba yatupasa tuchunguze kwa makini elimu tunayowapa watoto wetu. Ni wazi wakati umefika sasa tufikirie sana juu ya swali hili: 'Mpango wa Elimu katika Tanzania umewekwa kwa sababu gani – shabaha yake ni nini? Tutakapoamua hilo, tutazame kama muundo na elimu yenyewe inayopatikana Tanzania inafaa kwa kazi inayotakiwa kufanya. Kutokana na uchunguzi huo tunaweza kufikiri kama, kwa hali yetu ya leo, tunaweza kufanya mabadiliko zaidi, au kama kuna haja ya mapinduzi katika mpango mzima.

Twajaribu Kujenga Taifa la Namna Gani?

Tukifahamu bara bara aina ya Taifa tunalotaka kujenga, ndipo tutakapoweza kuweka mipango ya elimu yenye kutufikisha kwenye shabaha hiyo. Lakini hii si kazi kubwa katika Tanzania siku hizi. Ingawaje hatuwezi kusema kuwa tumekwisha weka mipango kamili ya maisha ya siku za mbele ya taifa hili. Lakini tumetamka mara nyingi haja na shabaha za taifa la ujamaa linalosimama juu ya nguzo tatu: usawa na heshima za binadamu; kushirikiana mali inayotokana

na juhudi zetu; kazi kwa kila mtu na kufuta unyonyaji. Tumezieleza fikara hizi waziwazi katika kanuni za taifa letu. Katika Azimio la Arusha na katika matamko mengine yaliyotangulia tumetaja misingi na siasa yetu na hatima ni umoja wa Afrika nzima, na kwamba tutafanya juhudi kufikia lengo hilo, lakini kwa sasa tutalinda heshima na uhuru wa Jamhuri ya Muungano. Na mara nyingi zaidi Serikali na watu wetu wamesisitiza usawa wa wananchi wote, na dhamiri yetu kufanya mipango ya uchumi, siasa na huduma zingine ilingane na usawa huo katika hali zote za maisha. Ndiyo kusema kwamba tumeamua maisha yetu ya baadaye yawe ya ujamaa ambayo watu wenyewe watapanga siasa itakayofuatwa na serikali iliyopata madaraka kutoka kwao.

Hata hivyo ni dhahiri kwamba, kama tunataka kupiga hatua kuelekea lengo hilo, sisi watu wa Tanzania hatuna budi tukubali hali yetu ya ndani ya nchi na hata nje, halafu tufanye bidii kuibadili hali hiyo ilingane na shabaha yetu. Na kweli ni kwamba Jamhuri yetu ya Muungano hivi sasa ni masikini, haijaendelea na uchumi wake mkubwa ni kilimo. Hatuna raslimali ya kutumia; tuna upungufu mkubwa wa watu wenye ufundi na wenye ujuzi katika viwanda vikubwa au mashine za kisasa. Vitu tulivyonavyo ni ardhi kwa wingi na watu walio radhi kufanya kazi kwa bidii kujiinua hali zao. Kufika ama kutofika katika lengo letu kunategemea tu matumizi yetu ya vitu na vitu hivyo viwili, ardhi na watu. Kama tutatumia amali hizo kwa moyo wa kujitegemea kuwa ndio msingi wa maendeleo yetu, basi tutapiga hatua yenye hakika, ingawa kwa taratibu. Na hayo ndiyo yatakayokuwa maendeleo ya kweli, yatakayoleta faida katika maisha ya umma na siyo maendeleo ya maonyesho tu katika miji, wakati watu wote wengine wa Tanzania wanaishi maisha yale yale ya ufukara tulio nao sasa.

Maana ya kuifuata shabaha hiyo ni kwamba kwa miaka mingi ijayo Tanzania itaendelea kupata uchumi wake kutokana na kilimo. Na kwa sababu watu wanaishi na kufanya kazi vijijini, basi hali ya maisha yanayostahili kuinuliwa ni ya watu wa vijijini. Tukisema hivi hatuna maana kwamba hatutakuwa na viwanda vipya katika siku za karibuni, la. Tunavyo viwanda hivi sasa na vitaendelea kukuzwa. Lakini litakuwa kama jambo la ndoto kuwaza kwamba katika siku chache zijazo sehemu kubwa ya watu wetu wataishi kwenye miji na kufanya kazi katika viwanda vya kisasa. Kwa hiyo hali ya vijiji haina budi kubadilishwa, viwe mahali ambapo watu wanaishi maisha mazuri. Watu hawana budi kupata utajiri utakaowaridhisha katika vijiji hivyo.

Lakini hali njema katika vijiji vyetu haitajileta yenyewe. Hali njema itakuja tu kama, kwa dhahiri tutafuata siasa ya kutumia kwa busara amali tulizonazo, yaani nguvu zetu na ardhi yetu. Maana yake ni kwamba watu wafanye kazi kwa bidii zaidi, wakitumia maarifa, na wafanye kazi pamoja; yaani wafanye kazi

kwa kushirikiana, watu vijijini na serikali yao pia, lazima wajiunge wajifanyie kazi wenyewe katika kijiji ambacho wao wenyewe ndio raia. Maisha yetu ya vijijini na mipango yetu ya serikali, lazima ifuate siasa ya ujamaa ambamo mna usawa wa kazi na mapato yatokanayo na jasho hilo.

Hivyo ndivyo inavyopasa mipango yetu ya elimu ifunze. Elimu yetu haina budi ipande mbegu ya watu kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote. Elimu haina budi iwaandae vijana wetu kutimiza wajibu wao katika kuendeleza vijiji vyao, ambamo wananchi wote wanashirikiana vyema kwa faida au hasara ya kijiji, na ambamo maendeleo yanapimwa kwa maisha bora, siyo kwa majumba ya fahari, magari, na vitu vingine, viwe vya watu binafsi au hata vya umma. Elimu yetu haina budi iwe ya kuwafunza vijana wajione kuwa ni sehemu ya jamaa, na kuwasaidia wanafunzi waelewe shabaha zetu za baadaye, siyo zile zilizokuwa zikitufaa siku zetu za zama za ukoloni.

Maana yake neno hili ni kwamba mipango ya elimu katika Tanzania haina budi kutilia mkazo juhudi ya pamoja siyo maendeleo ya mtu mmoja binafsi. Elimu haina budi kutilia mkazo mawazo ya usawa, na wajibu wa kuwahudumia wengine wakati mtu anao uwezo zaidi, kama ziada hiyo ni useremala, ufugaji, au hata elimu, na hasa, mipango yetu lazima ipinge majivuno ya elimu yanayowafanya wale waliosoma zaidi wawadharau wale walio na uwezo usiohitaji kusoma, au ambao hawana uwezo maalum, lakini ni binadamu. Majivuno ya namna hiyo hayana nafasi katika nchi yenye wananchi sawa.

Lakini mipango ya elimu yetu isiwe ya kufikiria usawa tu. Lazima vile vile iwekwe mipango ya kuwaandaa vijana wetu kwa kazi watakayotakiwa kufanya katika jamii ya Kitanzania: huko kijijini ambako maendeleo yatategemea sana kazi na juhudi za wakulima. Kusema hivi hatuna maana kwamba elimu ya Tanzania ipangwe katika namna ya kufunza wakulima wa aina mbali mbali wasiojua kufikiri, wanaofuata tu kama kondoo mipango na amri zote zinazotolewa na wakubwa. Lazima elimu hiyo izae wakulima bora, na vile vile iwaandae watu kushika madaraka wanayostahili, wakiwa wafanyakazi, wananchi huru, katika nchi huru ya kidemokrasi, ingawa ni ya wakulima. Hawana budi waweze kufikiri na kujiamulia mambo yote yanayohusu maisha yao; hawana budi waweze kuelewa uamuzi uliofanywa kidemokrasi katika vikao vinavyojulikana vya nchi yetu, na kutimiza uamuzi huo kwa kufuatana na mazingira ya mahali wanapoishi.

Kwa hiyo, kufikiria kwamba mipango yetu ya elimu iwe ya aina ya kufundisha madubwana tu, yanayofanya kazi kwa bidii bila kuuliza viongozi wa TANU na Serikali wanasema au kufanya nini, ni kutokuelewa haja yetu. Maana watu

ndiyo TANU na Serikali; lazima iwe hivyo. Serikali yetu, na Chama chetu, lazima wakati wote viwe na wajibu kwa watu, na lazima wakati wote viwe na wajumbe walio watetezi na watumishi wa watu. Kwa hiyo elimu tunayoitoa haina budi ihimize kila raia mambo matatu. Kwanza udadisi. Pili uwezo wa kujifunza kutokana na mambo ya watu wengine, na kukubali au kuyakataa mambo hayo kwa kupima haja zake mwenyewe. Na tatu, imani katika nafsi yake mwenyewe kwamba yeye ni raia katika jamaa hiyo aliye sawa na mwingine yeyote, anayewaheshimu wengine kama yeye mwenyewe anavyoheshimika, kutokana na kazi anazozifanya, wala si mapato apatayo.

Mambo haya ni muhimu kwa upande wa mafunzo ya kazi na pia kazi katika maadili ya maisha. Hata kijana akijifunza utaalamu wa kulima namna gani, hatapata kitabu kitakachompa majibu ya matatizo yote atakayoyakuta katika shamba lake mwenyewe. Itambidi ajifunze maarifa ya ukulima wa kisasa lakini halafu autumie ujuzi huo katika shamba, akitaka kuyafumbua matatizo yake. Kadhalika, wananchi huru wa Tanzania watapaswa wajiamulie wenyewe mambo yote yanayohusu maisha yao. Hakuna msahafu wa siasa, wala hautashuka msahafu, utakaotoa majawabu ya matatizo yote ya siasa ya uchumi yatakayotokea katika nchi hii katika siku za mbele. Yatakuwako mawazo na mipango itakayokubaliwa na nchi yetu, ambayo wananchi watafikiria na kutimiza kutokana na fikara zao na ujuzi wao wenyewe. Lakini mipango ya elimu katika Tanzania haitaifaidia nchi ya ujamaa ya kidemokrasi kama mipango hiyo itakuwa inawafanya watu wasithamini mafunzo, mipango na imani za viongozi wao, ama wa kale, ama wa sasa. Wanaoweza kujenga taifa huru ni watu huru wanaotambua utu na usawa wao.

Mipango ya Elimu ya Sasa

Shabaha yake mipango hiyo ni tofauti sana na shabaha tunayoilenga katika mipango yetu sasa. Maana kuna mambo manne makubwa katika mpango wetu wa sasa ambayo yanazuia au hayashawishi kukubalika kwa wanafunzi katika vijiji watakamoishi, na ambayo yanafunza fikara za ubwana, majivuno ya elimu na kujiona binafsi kwa vijana wanaopita katika shule zetu.

Jambo la kwanza kuhusu elimu tunayoitoa sasa ni kwamba elimu hii ni ya kibwana iliyopangwa kuwafaidia idadi ndogo sana ya watoto wanaoingia shule.

Ingawa vijana wetu watakaopata nafasi ya kuingia katika shule za sekondari ni 13 kwa mia tu ya wale wanaokwenda shule za misingi, lakini hata hivyo mpango wa shule zetu za msingi ni wa kuwatayarisha watoto wetu kuingia katika shule

za sekondari. Kwa hiyo 87 kwa mia ya watoto wetu waliomaliza shule mwaka uliopita na wengine kama hao watakaomaliza mwaka huu, wanaondoka shuleni wakifikiri kwamba wameshindwa, na kukoseshwa matumaini yaliyokuwa haki yao. Na kwa kweli, wote sisi tunasema vivyo hivyo, tunawaita vijana hawa kama 'wale walioshindwa kuingia shule ya sekondari', badala ya kuwaita 'vijana waliomaliza elimu ya msingi'. Na kwa upande mwingine, wale 13 kwa mia wanaendelea kuwa na fikara ya kustahili tuzo, na tuzo wanalolitumaini wao na wazazi wao ni mishahara mikubwa, kazi za raha mijini na jina kubwa mitaani. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa wale wanaopanda ngazi ya juu zaidi, wakati wanapoingia Chuo Kikuu.

Ndiyo kusema kwamba elimu inayotolewa sasa ni kwa ajili ya wachache tu wenye uwezo wa mitihani kuwazidi wengine; inawafanya wale wanaofanikiwa wajione kuwa wakubwa, na kuwafanya wale walio wengi wakitamani kitu ambacho hawatakipata daima. Inawafanya walio wengi wajifikirie kuwa wanyonge na kwa hiyo hawawezi kuunda wala taifa la usawa tunalotaka kulijenga wala fikara zinazoelekea kwenye taifa lenye usawa. Kinyume chake, elimu hiyo inashawishi kuundwa kwa taifa lenye tabaka, la ubwana na utwana, katika nchi yetu.

Jambo la pili ni muhimu vile vile, nalo ni kwamba elimu ya Tanzania inawatenga wale wanaosoma mbali na wananchi wanaowasomesha. Hii ni kweli hasa kwa shule za sekondari ambazo karibu zote ni za wanafunzi kukaa huko shuleni. Lakini ni kweli vile vile hata katika shule chache za praimari, ijapokuwa hivi karibuni tumebadili kidogo mipango yetu.

Tunawachukua watoto wakiwa na umri wa miaka 7 kutoka kwa wazazi wao, na tunawafunza masomo ya darasani saa 7 1/2 nzima kutwa. Katika miaka michache iliyopita tumejaribu kuyafanya mafunzo haya yafanane na hali ambayo watoto hao wanaiona. Lakini shule yenyewe kila mara iko mbali, siyo karibu na jamaa au kijiji. Shule ni mahali ambapo watoto huenda kwa matumaini, yao na wazazi wao, kwamba wakifanikiwa haitakuwa lazima kwao kuwa wakulima au kuishi vijijini.

Wale wachache wanaoingia shule za sekondari hupelekwa mbali na makwao, wanaishi maisha ya pekee, wakiwa na ruhusa ya kwenda mjini kujistarehesha, lakini kazi za mji au kijiji kile hazilingani na maisha yao hasa, yaani maisha wanayoishi wakiwa katika uwanja wa shule. Baadaye wachache huenda Chuo Kikuu. Wakiwa na bahati kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaishi katika nyumba za raha, wanalishwa vizuri na kusoma sana kupata digrii zao. Watakaopata digrii hiyo wanajua mara moja kwamba watapokea mshahara kiasi

cha shilingi 1,100/- kwa mwezi. Hiyo ndiyo shabaha waliyokuwa nayo, ndiyo waliyofunzwa wawe nayo. Wanaweza vile vile kuwa na haja ya kuuhudumia umma, lakini fikara zao za huduma zinatokana na heshima na mshahara ambao mtu aliyehitimu Chuo Kikuu anaweza kuupata. Mshahara na hadhi vimekuwa haki inayotolewa na Digrii.

Tutakosea tukiwalaumu vijana wetu kwa fikara kama hizi. Kijana aliyehitimu sasa hivi kutoka Chuo Kikuu ametumia sehemu kubwa ya maisha yake mbali kabisa na watu wa Tanzania. Inawezekana wazazi wake ni maskini, lakini yeye kwa kweli hakuonja umaskini ule. Hafahamu maisha ya mkulima maskini hasa yako namna gani. Ataona raha zaidi kuishi na watu wenye elimu, kuliko kuishi na wazazi wake mwenyewe. Kijana huyu amekwenda nyumbani wakati wa likizo tu, na hata wakati huo wazazi na jamaa zake wenyewe wamesisitiza fikara zake za ubwana, na kudhani kwamba ni makosa yeye kuishi na kufanya kazi kama mtu wa kawaida. Maana kweli ni kwamba watu wengi wa Tanzania wamehesabu mtu mwenye elimu kuwa wa thamani sana hata hawezi kuishi maisha ya taabu wanayoishi watu wetu wengine.

Jambo la tatu ni kwamba mpango wetu wa elimu wa sasa unawafanya wanafunzi wafikiri kwamba mambo yote ya maana hupatikana katika vitabu, au hutoka kwa 'watu wenye elimu', yaani wale waliopata elimu ya darasani. Ujuzi na hekima ya wazee wengine hudharauliwa, na wao wenyewe hujihesabu kuwa maamuma wasiofaa lolote. Kwa kweli si mpango wa elimu peke yake unaoleta mawazo kama hayo. Hata Serikali na Chama pia huwachagua watumishi kwa kufuata 'School Certificate' au digrii, na kadhalika. Kama kijana anazo hati hizo tunadhani kwamba anaweza kufanya kazi fulani. Hatungojei tukamjua mawazo yake, tabia yake, au uwezo wake mwingine, midhali tu amefaulu katika mtihani. Kama mtu hana hati hiyo tunadhani kwamba hawezi kuifanya kazi, tunasahau kabisa habari ya ujuzi na mazoea yake ya kazi. Kwa mfano, hivi juzi juzi nilimtembelea mwananchi mmoja, mlima tumbaku hodari sana. Lakini kama ningejaribu kumwajiri mtu huyu Serikalini awe Bwana Shamba wa tumbaku ningekwama, maana hana hati ya kusomea darasani. Kila kitu tufanyacho kinatilia mkazo masomo ya darasani, na kudharau sana hekima ambayo mara kwa mara huipata watu wanaotumia akili, waume kwa wake, jinsi wanavyoendelea kuishi, hata kama hawawezi kusoma au kuandika.

Kusema hivi maana yake siyo kwamba mtu yeyote anaweza kufanya kazi yoyote, mradi tu amekuwa mwenye hekima, wala si kusema kwamba hati za elimu si lazima. Wakati mwingine watu wetu wamefanya makosa ya kufikiri hivyo kwa sababu tu ya kuchukia majivuno ya wale wenye elimu. Mtu hawi na busara tu kwa sababu ni mzee; mtu hawezi kuendesha kiwanda kwa sababu

tu ameajiriwa kama kibarua au mtunza stoo kwa muda wa miaka 20 iliyopita. Lakini vile vile pengine atashindwa kufanya kazi hiyo hata akiwa na digrii ya biashara. Huyu wa kwanza anaweza kuwa na uaminifu na uwezo wa kusimamia wenzake, huyu wa pili huenda ana uwezo wa kuanzisha na kupanga hesabu zake. Lakini, kama tunataka kiwanda hiki kifanikiwe, kiwe cha kisasa, na kulifaidia Taifa, basi meneja anatakiwa awe na sifa zote hizi mbili. Ni makosa vile vile kufikiria kisomo ndicho kila kitu.

Na hivyo ndivyo ilivyo katika ujuzi wa kilimo. Wananchi wetu ni wakulima wa siku nyingi. Ufundi wanaoutumia ni matokeo ya juhudi ya miaka mingi ya kutafuta riziki; na hata sheria na miiko wanayoifuata ina sababu zake. Haitoshi kumkashifu mkulima mzee kwa kudhani kuwa anatumia maarifa ya kale. Hatuna budi kujaribu kufahamu kwa nini anafanya mambo fulani, tusidhani tu kuwa ni mpumbavu. Wala sisemi kwamba maarifa yake yanafaa katika siku zijazo. Inawezekana kuwa maarifa ya asili yalifaa kwa siku zile yalipotumiwa, kufuata ujuzi uliokuwapo. Lakini siku hizi tunatumia vifaa tofauti, na tuna mipango tofauti ya kumiliki ardhi. Haiwezekani sasa kulima shamba kwa muda wa mwaka mmoja au miwili, na halafu kulitelekeza kwa muda wa miaka 20, ili rutuba irudi tena. Kutumia plau la ng'ombe badala ya jembe, au hata kutumia trekta katika sehemu zingine, maana yake siyo peke yake kubadili namna ya kulima. Yatakiwa yawepo mabadiliko katika mpango wa kazi, ili kuhakikisha kwamba chombo hiki kipya kinalima kwa faida zaidi, na pia maarifa haya mapya hayaharibu kwa haraka ardhi yetu wala misingi ya usawa ya taifa letu. Kwa hiyo nasisitiza tena kwamba vijana wetu hawana budi wajifunze kuheshimu hekima ya wakulima wazee wasiosoma, na kuelewa maarifa ya kisasa, na kwa nini maarifa hayo yatatumika.

Lakini ilivyo sasa ni kwamba vijana wetu wanajifunza kuwadharau hata wazazi wao, kwa sababu tu mambo yao ni ya kizamani na hawakusoma. Hakuna kitu chochote katika mipango yetu ya elimu kinachomwelekeza mwanafunzi kwamba anaweza kujifunza mambo ya maana kuhusu kilimo kutoka kwa wazee wake. Matokeo yake ni kwamba anapagawa na imani za uchawi kabla hajaenda shule, lakini hajifunzi aina za dawa za porini; anajifunza miiko ya ukoo wake lakini hajifunzi jinsi ya kupika chakula cha kufaa mwili kwa ufundi wa kiasili. Na akitoka shule anapata masomo yasiyofanana kabisa na maisha ya kilimo. Kwenye utaalamu hajafikia na kwenye ukulima hayuko.

Na jambo la mwisho na kwa sababu nyingi ndilo muhimu zaidi, taifa letu changa na masikini linawasamehe baadhi ya vijana wake wenye nguvu na afya kabisa, wasifanye kazi zenye kuleta maendeleo nchini. Wanashindwa kuongeza uchumi unaotakiwa sana na taifa letu; na zaidi ya hapo wao wenyewe wanakula tu nguvu

za wazee na watu wengine walio wanyonge zaidi. Hivi sasa tuna wanafunzi wapatao 25,000 katika shule za sekondari. Hawa hawajifunzi kwa kufanya kazi; wanasoma tu. Je bado wanaamini tu kuwa hii ndiyo haki yao. Katika nchi tajiri kama Amerika ni jambo la kawaida kabisa kwa kijana kufanya kazi na kujilipia gharama za masomo katika vyuo vikuu, lakini katika Tanzania mipango yetu ya elimu haiwapi nafasi wanafunzi kufanya hivyo. Hata wakati wa likizo tunaona kwamba vijana hawa wa kike na wa kiume wanapaswa walindwe wasifanye kazi ngumu. Wao wenyewe, na hata watu wa vijiji vyao, hawawatarajii kutumia wakati wao wakifanya kazi ngumu kwa mikono yao au kufanya kazi za karaha na zisizopendeza. Hii haidhihirishi tu kwamba kuna watu wengi wanaotafuta kuajiriwa kazi, maana ujira siyo ugomvi, kwa sasa inadhihirisha aina ya mawazo ambayo sisi tumeyakubali.

Wanafunzi wetu wangapi wamediriki kutumia siku zao za mapumziko kufanya kazi ambazo zitainua hali ya maisha ya watu, bila ya malipo; kazi kama vile kuchimba mifereji ya kumwagilia maji mashambani au ya kuondoa maji kijijini, au kuelekeza jinsi ya kuchimba choo na faida zake, na kadhalika? Idadi ndogo ya wanafunzi wamefanya kazi hizo katika kambi 55 Elimu ya Kujitegemea za vijana au kwa mpango wa kujenga Taifa ulioanzishwa na shule nzima, lakini hii si kawaida. Walio wengi hawafikirii ujuzi wao au nguvu zao kuwa zinahusiana na haja za kijiji kizima.

Je, Makosa Haya Yanaweza Kurekebishwa?

Kama tunataka hali hii ibadilike, kuna mambo matatu yanayopaswa kufikiriwa. Kwanza mafunzo yenyewe yanayotolewa, pili mipango ya shule, na tatu umri wa watoto kuanza shule. Ingawa mambo hayo yanaonekana kuwa tofauti, lakini yanahusiana sana. Hatuwezi kuwaunganisha wanafunzi na taifa lao la baadaye kwa mafunzo ya vitabuni tu, hata kama mafunzo hayo ni mazuri namna gani. Wala taifa haliwezi kufaidika na mpango wa elimu unaohusiana kabisa na maisha ya kijijini, lakini mpango huo hauwafundishi watoto masomo ya lazima kama vile kusoma na hesabu, au hauwafanyi wawe wadadisi katika mawazo yao. Wala hatuwezi kuwatarajia wale wanaomaliza mafunzo yao katika shule za msingi kuwa raia wa manufaa, kama umri wao wakati huo ni miaka 12 au 13 tu.

Tunapofikiria mabadiliko ya mtindo wa sasa ni muhimu vile vile tutambue hali yetu ya uchumi ilivyo. Kila senti tunayotumia katika elimu ni fedha tunayoiondoa katika kazi nyingine, tunaweza tukaiondoa kutoka mpango wa maendeleo, au hospitali, au hata chakula, nguo na starehe za wananchi wengine wa sasa. Na kweli ni kwamba hakuna uwezekano wa Tanzania kuongeza

gharama zinazotumiwa katika elimu; haki yake gharama hizo zipunguzwe. Kwa hiyo hatuwezi kuondoa tatizo letu la sasa kwa njia yoyote itakayoligharimu taifa zaidi kuliko ilivyo sasa. Na hasa hatuwezi kuondoa tatizo la vijana wanaomaliza masomo ya msingi kwa kuongeza nafasi katika shule za sekondari.

Kwa kweli tatizo la vijana waliomaliza shule za msingi linaletwa na mpango wetu wa sasa wa elimu. Zaidi na zaidi watoto wanaanza masomo wakiwa wadogo mno, miaka sita, hata mitano, na hivyo wanamaliza darasa la saba wakiwa wadogo mno kuweza kufanya kazi yoyote ya maana. Juu ya hivyo masomo aliyopata yanalifanya taifa na mtoto huyu ategemee kupata kazi za kuajiriwa; kama vile ukarani. Ndio kusema kwamba elimu yao haikulingana vya kutosha na kazi watakazotakiwa kuzifanya katika taifa. Tatizo hilo linatulazimu tufanye mabadiliko makubwa ya aina ya mafunzo katika shule za msingi, na kuchelewesha watoto kuanza shule ili atakapomaliza masomo yake mtoto awe mkubwa wa kutosha. Hakuna njia nyingine ya kuondoa tatizo hili la watoto waliomaliza darasa la saba. Ijapo tatizo hilo linauma, lakini kweli ni kwamba miaka mingi itapita kabla Tanzania haijaweza kuwapa watoto wote elimu ya msingi. Na kwa walio wengi wa wale wanaopata nafasi hizo, elimu yao itakuwa sawa na madarasa saba ya sasa. Ni wachache tu watakaopata nafasi ya kwenda shule za sekondari, na karibu sasa wachache zaidi wa wale watakaoingia shule za sekondari watapata nafasi ya kuingia chuo kikuu, hata kama wana akili na uwezo wa kuendelea na masomo hayo. Hiyo ndiyo hali yetu ya maisha na uchumi wa nchi yetu. Hiyo ndiyo maana ya umasikini wetu. Tunaloweza kufanya tu ni jinsi ya kuzigawa nafasi za elimu; kama tutasisitiza faida ya wachache, au kama tunaweka mipango ya elimu iwe yenye faida kwa taifa zima. Na katika nchi ya ujamaa, linalowezekana tu ni kuwa na elimu ya manufaa kwa taifa zima.

Maana ya maneno haya ni kwamba elimu tunayoitoa katika shule za msingi lazima iwe elimu inayotutosheleza. Isiendelee kuwa elimu ya kuwandaa watoto kwenda shule za sekondari. Badala ya kupanga kazi za shule za msingi zielekee kwenye mashindano ya mtihani utakaochagua wachache wao tu kuingia katika shule za sekondari, sasa mipango iwe ya maandalio ya aina ya maisha ambayo vijana walio wengi wataishi. Kadhalika, shule za sekondari zisiwe tu mahali pa kuchagulia vijana kuingia Chuo Kikuu, vyuo vya elimu, na kadhalika. Shule hizo hazina budi ziandae vijana kwa kazi katika vijiji na sehemu za mashambani za nchi hii. Maana katika Tanzania sababu peke yake ya kuwapa wachache elimu ya sekondari ni kwamba wanaihitaji ili waweze kuwatumikia walio wengi. Mwalimu katika shule ya msingi ana haja ya elimu iliyozidi darasa la saba; Bwana Shamba atakayewasaidia wananchi wenye elimu ya darasa la saba yeye mwenyewe anapaswa awe na elimu kubwa zaidi. Huduma nyingine

zilizo za lazima zinahitaji elimu ya juu zaidi, kwa mfano madaktari na mainjinia wanahitaji mafunzo ya miaka mingi. Lakini elimu ya kawaida inayotolewa na taifa haina budi iwe elimu ya umma. Hakuna sababu nyingine inayotupa haki kuwatoza walio wengi na kuwapa elimu wachache tu.

Hata hivyo, ni rahisi kutamka kwamba masomo katika shule za msingi na sekondari hayana budi yawaandae vijana kwa maisha na haja za Tanzania. Lakini kutimiza kunataka mapinduzi, si mapinduzi ya mipango ya elimu peke yake, bali hata ya fikara za sasa za wananchi. Na hasa, mitihani inapaswa ibadiliwe ifanane na mawazo ya serikali na ya wananchi. Sharti tufahamu kwamba ingawa mitihani ina faida zake, kama vile kupunguza hatari za upendeleo na ukabila katika kuchagua watakaoendelea, mitihani ina hasara kubwa pia. Kwa kawaida mitihani inapima uwezo wa mtoto, kujifunza mambo na kuyaeleza kwa muda fulani wakati anapotakiwa. Mitihani haifanikiwi siku zote kupima uwezo wa mtoto kufikiri, na hakika hauwezi kupima tabia wala ridhaa ya utumishi.

Kadhalika, kwa sasa mafunzo hutolewa kufuatisha mitihani itakayotolewa; ni shida kubwa mitihani kutungwa kutokana na mafunzo. Mwalimu anayejaribu kuwasaidia wanafunzi wake mara kwa mara husoma maswali ya mitihani iliyopita, na kubuni maswali gani yanaweza kutokea safari hii. Basi mafunzo yale anayakazania pale pale, akijua kwamba kwa kufanya hivyo anawapa wanafunzi wake nafasi nzuri ya kufaulu na kuingia katika shule za sekondari, au Chuo Kikuu. Na mitihani yenyewe wanayofanya watoto wetu sasa inatungwa kufuata mahitaji na mazoea ya mataifa mengine; inapangwa bila ya kufikiria shida au haja zetu maalum. Tunalotaka kufanya sasa ni kufikiria kwanza elimu tunayotaka kuitoa, na baada ya hapo tufikirie aina gani ya mitihani inafaa katika kumaliza masomo hayo. Hapo mtihani huo utatungwa kufanana na mafunzo yaliyotolewa.

Jambo kubwa zaidi ni kubadili mambo tunayotaka yatendeke shuleni. Mambo wanayofundishwa watoto wa shule za msingi yasipangwe kutokana na mambo anayotaka kuyajua daktari, injinia, mwalimu, mtaalamu uchumi au Bwana Shauri. Watoto wetu walio wengi hawatafanya kazi hizo kamwe. Mambo wanayofundishwa watoto wa shule za msingi yawe yale ambayo wavulana na wasichana wanapaswa kuyajua, yaani ufundi wa kazi anayotakiwa afanye na maadili anayotakiwa awe nayo ili aishi vyema na kwa furaha katika nchi ya ujamaa ambayo ni ya wakulima na kusaidia kuinua hali ya maisha ya kijiji chake. Macho yetu yawatazame walio wengi, hao ndio tuwafikirie tunapoamua masomo gani yafundishwe. Wale watakaofaa kwa masomo ya juu zaidi bado watajitokeza, na wala hawatapata taabu yoyote. Maana shabaha yetu siyo kutoa elimu hafifu kuliko ile inayotolewa sasa. Shabaha ni kutoa elimu ya aina tofauti,

ya masomo yanayopangwa kutimiza shabaha ya umma, ya elimu itakayolifaa taifa la Tanzania. Na hivyo hivyo katika shule za sekondari. Shabaha ya mafundisho iwe kutoa elimu, ufundi na fikara ambazo zitamfaa mwanafunzi wakati atakapoishi katika nchi ya kijamaa inayobadilika; shabaha yake isiwe kuingiza wanafunzi katika Chuo Kikuu.

Pamoja na mabadiliko haya ya mipango ya masomo yenyewe, lazima yaweko vilevile ya jinsi shule zetu zinavyoendeshwa, ili kuzifanya shule hizo, pamoja na wanafunzi wake kuwa sehemu ya kijiji na sehemu ya uchumi wa nchi. Kwa kweli shule zapaswa ziwe kama jamaa kamili, zinazoishi kufuata Siasa ya Kujitegemea. Walimu, wafanya kazi wengine, na wanafunzi lazima, kwa pamoja, waishi kama jamaa, kama vile vile ambavyo wazazi, ndugu na watoto wanakaa katika jamaa moja. Uhusiano baina ya walimu na wanafunzi katika shule, lazima uwe wa aina ile ile kama wazee na watoto wote waishivyo kijijini. Shule itambue, kama vile vile jamaa inavyotambua, kwamba maisha na hali zao zitategemea wao wenyewe watakavyotafuta mali kwa kilimo au kwa kazi zingine. Maana yake ni kwamba shule zote, lakini hasa shule za Sekondari na Vyuo vya Juu, lazima zijitafutie zenyewe chakula. Shule hizo hazina budi zikamilike katika mambo ya uchumi, huduma na elimu kadhalika. Kila shule ingepaswa iwe na shamba lake au Kiwanda chake, kama sehemu kamili ya shule, linalotoa chakula cha kutumiwa na watu wote shuleni, na wakati huo huo kusaidia kuongeza uchumi wa Taifa zima.

Kusema hivyo maana yake siyo kwamba kila shule lazima iwe na shamba au Kiwanda cha kufundishia. Wazo ni kwamba kila shule iwe shamba vile vile, yaani shule iwe na wakuu ambao ni walimu na wakulima kadhalika, na iwe na wanafunzi ambao ni wakulima kadhalika. Ni dhahiri, kama kuna shamba la shule, wanafunzi wanaolima humo watakuwa wakijifunza kazi na ufundi wa kulima. Lakini shamba lenyewe litakuwa sehemu ya shule, na hali ya wanafunzi itategemea mazao ya shamba hilo, kama vile vile ambavyo hali ya mkulima inategemea mazao ya shamba lake. Kwa hiyo wakati mpango huu utakapokuwa unaendelea vema, mapato ya shule hayatatokana na fedha za Serikali Kuu tu, au fedha kutoka misheni, au msaada wa watu wengine. Wakati huo daftari la mapato ya shule litaonyesha kama: 'Kuuza pamba (au mazao mengine yoyote yanayopatikana katika shamba hilo) Shilingi kadha'; mwishowe ndio 'Msaada wa Serikali na msaada kutoka sehemu zingine Shilingi kadha'.

Haya ni mapinduzi ya mipango ya elimu tuliyoizoea, na kama walimu na wazazi hawaelewi vema shabaha na uwezekano wa jambo hili, mpango huu unaweza ukapingwa mwanzoni. Lakini kweli ni kwamba hii si hatua ya kurudi nyuma, wala si adhabu kwa walimu au kwa wanafunzi. Ni kukubali tu kuwa sisi watu wa Tanzania tutajiondoa kutoka hali ya umasikini wetu kwa kazi zetu, na kwamba sote sisi ni viungo vya Taifa moja tunaotegemeana. Kutakuwako shida

za kutimiza jambo hili, hasa hapo mwanzo. Kwa mfano hatunao sasa mabwana shamba wa kutosha ambao wangeweza kupanga kazi za ukulima na kuangalia mashamba katika shule. Maisha na ukulima yataendelea vivyo hivyo kwa jinsi tunavyojifunza. Na kwa kweli tunaweza kuondoa zile fikara kwamba elimu sharti ipatikane kitabuni, kama tutawatumia wakulima mahodari wa vijijini kama waalimu na waangalizi wa kazi fulani, na kuwatumia mabwana shamba kama wasaidizi tu. Hili ni jambo muhimu katika maendeleo yetu ya ujamaa.
Wala fikara za shule kujitafutia chakula chao wenyewe hazina maana kwamba tutatumia watoto wetu kama vibarua, wanaofanya kazi kwa kufuata maarifa ya kizamani tu. Kinyume chake, wanafunzi wetu katika shamba la shule watajifunza kwa kufanya kazi. Kazi ya jembe na vifaa vingine itafundishwa; vile vile faida ya kuchagua mbegu, faida ya kutumia plau la ng'ombe, na faida za kutunza mifugo vizuri zitaonekana. Na watoto watajifunza kwa vitendo jinsi ya kuvitumia vifaa hivyo kwa faida. Kazi ya shamba, mazao ya shamba, yaunganishwe kabisa na maisha ya shule. Kwa hiyo kazi za mbolea aina mbali mbali zinaweza zikaelezwa darasani, lakini jinsi ya kutumia mbolea hizo, na shida zake, mtoto anajifunza wakati anapoona mbolea zinatumiwa. Jinsi ya kuwalisha ng'ombe vizuri, kulima matuta, na maarifa ya kuzuia mmomonyoko wa udongo, yote haya yanaweza kufundishwa darasani, lakini wakati huo huo mtoto hujifunza kwa vitendo. Hapo wanafunzi wataelewa vitu wanavyofanya na sababu zake; wanaweza kufafanua hitilafu na kugundua njia za kurekebisha hitilafu hizo.

Lakini shamba la shule lisiwe shamba kubwa kama maonyesho tu, la kulima kwa trekta. Na kwa kweli haliwezi kuwa hivyo. Hatuna fedha wala vyombo vinavyotakiwa kulifikisha shamba katika hali hiyo, na wala halitawafundisha wanafunzi lolote kuhusu maisha watakayoishi baadaye. Shamba la shule lazima lianzishwe na watu wote wa shule hiyo, wao wenyewe wakifyeka msitu, na kufanya kazi zingine lakini kwa pamoja. Kwa njia hiyo watoto watajifunza faida ya juhudi za pamoja, hata kama haukupatikana msaada mkubwa wa fedha kutoka nje. Vile vile faida za kushirikiana zinaweza kufunzwa darasani na kuonyeshwa shambani.

Jambo lililo muhimu zaidi ni watu wote wa shule ile watambue kwamba shamba hilo ni lao, na hali yao ya maisha itategemea shamba hilo. Wanafunzi lazima wapewe nafasi ya kuamua mambo mengi yanayolihusu shamba hilo: kwa mfano, kama inafaa kutumia fedha walizozipata kukodishia trekta ili liwatayarishie shamba kabla ya kupanda au kama inafaa kutumia fedha hiyo kwa kazi zingine katika shamba au katika shule, au kama wataendelea kufanya kazi ngumu wao wenyewe kwa mikono yao. Kwa njia za namna hii, na kwa kuunganisha masomo ya darasani na ya shambani, watoto wetu watajifunza kwamba kama wakilima vizuri basi watakula vizuri, na watakuwa na vifaa vizuri katika mabweni yao, katika nyumba za mapumziko na kadhalika. Na kama wakilima vibaya basi

wao wenyewe ndio watakaopata taabu. Katika jambo hili Serikali lazima iache kuweka sheria na maagizo mengi. Kila shule lazima iwe na mipango yake. Kwa njia hiyo tu ndipo tunavyoweza kutumia nafasi zilizopo kila mahali, na kwa njia hiyo tu ndivyo wanafunzi watakavyoweza na kuheshimu demokrasi.

Kwa njia hiyo wanafunzi wetu wataweza kujifunza kuwa starehe hutokana na kazi. Watajifunza maana ya kuishi pamoja na kufanya kazi kwa faida ya wote, na vile vile faida ya kushirikiana na watu wa kijijini wasiokuwa wa shule ile. Maana watatambua kwamba vitu vingi vinahitaji juhudi za watu zaidi kuliko wa shule ile tu. Watatambua kwamba wakishirikiana na wakulima wa kijiji wanaweza kuleta mifereji ya kumwagilia maji shamba lao. Watajifunza kwamba ili maendeleo yapatikane mtu hana budi achague ama ajifurahishe sasa ama ajifurahishe baadaye; kila mtu binafsi na kijiji pia.

Pengine mwanzoni makosa yatafanywa, na kwa kweli si vyema kuwapa uhuru kabisa wanafunzi tangu mwanzo. Lakini ingawa uongozi lazima utolewe na wakuu wa shule, na ingawa wanafunzi wanapaswa wawekewe masharti, wanafunzi wenyewe lazima waweze kufanya uamuzi, na wafanyapo makosa watajifunza. Kwa mfano, waweza wakajifunza kuweka daftari ya shamba la shule, ambamo huandikwa kazi zinazofanywa, mbolea zinazotumiwa au chakula walicholishwa ng'ombe, n.k., na idadi ya mazao kutoka katika kila sehemu ya shamba. Hivyo wanaweza kusaidiwa kuona mahali gani panataka mabadiliko, na kwa sababu gani. Maana ni muhimu vile vile kwamba mambo ya mipango yafundishwe darasani na kuonyeshwa shambani pia. Shule nzima iungane kuweka mipango ya kazi ya mwaka mzima, na kugawana wajibu na kupanga tarehe za kazi mbalimbali katika mpango mzima. Vikundi mbalimbali vya shule huenda vikapata faida zaidi, kutokana na jinsi walivyotimiza kazi waliyopangiwa, lakini iwe baada ya watu wengine wote wa shule ile kupokea mazao yanayostahili katika maendeleo. Mipango ya namna hii vile vile ni mafunzo ya ujamaa.

Kama shule iko kijijini (na katika shule mpya zitakazojengwa siku zijazo) itawezekana kwamba shamba la shule liwe karibu karibu na shule yenyewe. Lakini katika miji na katika shule za zamani zilizo katika vijiji vyenye watu wengi, huenda isiwezekane kuwa hivyo. Katika hali hiyo shule inaweza kutilia mkazo kazi zingine zenye kuleta uchumi, au inawezekana katika shule za mabweni wanafunzi wakatumia sehemu ya mwaka darasani, na sehemu nyingine katika kambi ya shamba lao lililo mbali. Kila shule itafanya mpango wake. Itakuwa makosa kuzisamehe shule za mijini, hata kama watoto huja shule kila siku, wasitimize mpango huu mpya.
Kazi nyingi ambazo sasa wanafanyiwa wanafunzi, hasa wale walio katika shule za Sekondari, zapasa zifanywe na wanafunzi wenyewe. Kwanza, mtoto

anayeingia shule akiwa na umri wa miaka saba, atakuwa na umri wa miaka 14 akiingia shule ya Sekondari, na umri wa miaka 20 na 21 amalizapo. Lakini katika shule zetu nyingi sasa tunaajiri shamba boi, siyo kuwafunza watoto kazi, bali kuifanya kazi ile badala ya watoto wenyewe. Wanafunzi wanakua na mawazo ya kuandaliwa chakula chao na watumishi, na kuoshewa sahani, kufagiliwa vyumba, na bustani zao kuangaliwa. Hata kama wakiombwa kusaidia katika kazi hizi wanaona unyonge, na kufanya kidogo kadiri inavyowezekana, na kama mwalimu yupo anawaangalia. Hii ni kwa sababu hawakujifunza kujivunia chumba safi na bustani nzuri, kama vile wanavyojivunia insha safi na hesabu walioifanya vizuri. Lakini je, haiwezekani kazi hizi zikaunganishwa katika jumla ya mafunzo ya shule? Ni lazima Mwalimu Mkuu na makarani wake watumie muda mrefu kuandika waranti za kusafiria watoto wakati wa likizo? Haiwezekani hata moja ya kazi hizi zikafundishwa darasani, ili watoto wajifunze kufanya kazi hizi wenyewe? Yaani, haiwezekani hata shule za sekondari, zikawa zinazojitosheleza kiasi chake, ambako waalimu na waangalizi wanaletwa kutoka sehemu zingine, bali kazi zingine zinafanywa ama na jumuia nzima ya shule au kulipiwa gharama ya pamoja? Ni kweli kwamba kwa wanafunzi shule ni mahali pa kupita tu, lakini hapa ndipo patakapokuwa kwao kwa muda wa miaka saba mizima.

Ni dhahiri kwamba hali kama hiyo haiwezi kufikiwa kwa siku moja. Kunahitajiwa mabadiliko makubwa ya mipango na mafunzo, na kwa hiyo mabadiliko hayo hayana budi kuletwa pole pole, kila miezi inavyopita mashule yachukue pole pole madaraka zaidi ya kujitosheleza. Wala haitegemei kwamba watoto wa shule za msingi wanaweza kujitosheleza sana wenyewe, ingawaje yatupasa kukumbuka kuwa wale wakubwa watakuwa na umri wa miaka 13 na 14, umri ambao watoto katika nchi nyingi za Ulaya huwa tayari wanafanya kazi.

Lakini ingawa shule za msingi haziwezi kutarajiwa kujitegemea kama shule za sekondari, ni muhimu kabisa kwamba shule hizo, na wanafunzi wao, ziwe na uhusiano kamili na maisha ya vijijini. Wanafunzi lazima waishi kama sehemu ya jamaa ya uchumi kwa kuwa na wajibu katika jamaa hiyo, na kukifanya kijiji kishiriki katika mambo ya shule. Vipindi vya mwaka wa shule, na vipindi vya darasani, vyote vipangwe katika namna itakayowawezesha wanafunzi, kama watu wa jamii, na watoto wa kijiji, washiriki kazi katika shamba la jamii la kijiji. Kwa sasa watoto wasiokwenda shule wanalima shambani kwa baba au katika shamba la ushirika, au wanachunga ng'ombe; hiyo ni lazima kwao. Yapasa liwe jambo la lazima vile vile watoto wanaosoma shule waweze kushiriki katika kazi za jamaa, si kwa kupendelewa au kwa hiyari wakati tu wanapotamani kunyoosha maungo, lakini kama sehemu ya kawaida ya malezi yao. Mtindo wa sasa wa kuihesabu shule kuwa ni kitu cha pekee, na wanafunzi kama watu

wasiolazimika kufanya kazi, hauna budi uachwe. Katika jambo hili wazazi wana wajibu maalum, lakini shule pia zinaweza kusaidiana sana kuunda mawazo haya mapya.

Kuna njia nyingi tofauti za kuufikia uhusiano huo. Lakini lazima watoto watambue kwamba wanaelimishwa na umma ili wawe raia wenye akili na bidii kutimiza wajibu wao katika umma. Njia moja inayowezekana ya kufanya hivi ni kuleta katika shule za msingi mpango wa kujifunza kwa vitendo kama vile vile inavyoshauriwa iwe katika shule za sekondari. Kama watoto wa shule za msingi wanafanya kazi katika shamba la ushirika la kijiji, tuseme wamegawiwa kipande chao maalum kukiangalia, basi watajifunza maarifa mapya ya kilimo na kujivunia mafanikio ya shule yao. La kama hakuna shamba la ushirika kijijini basi shule inaweza kuanzisha shamba lao wenyewe kwa kuwaomba wale walio wakubwa zaidi wafyeke misitu wakati watoto wengine wanapofanya kazi nyingine za jumuiya.

Kadhalika iwapo kazi za maendeleo, kama vile majumba mapya na vitu vingine vinatakiwa katika shule, basi wanafunzi na wakazi wa kijiji washiriki pamoja, wakigawana kazi zinazolingana na afya na nguvu za kila mmoja wao. Watoto wa shule, wavulana kwa wasichana, yawapasa waangalie usafi wao wenyewe, na wajifunze faida ya kufanya kazi pamoja, na ya kuweka mipango ya maisha ya baadaye. Kwa hiyo, kama wana shamba lao wenyewe, watoto watahusika katika kazi tu bali vile vile katika ugawaji wa mazao yanayopatikana, na ya kula na ya kuuza pia. Hawana budi washiriki katika kuchagua baina ya faida za shule na faida za kijiji, na baina ya faida ya sasa na faida ya baadaye. Kwa njia hizi na zingine watoto hawana budi, wajifunze tangu mwanzo mpaka mwisho wa mafunzo yao, kwamba elimu haiwatengi, bali inawasaidia kuwa raia wenye faida katika kijiji, kwa faida zao wenyewe na kwa faida ya taifa zima na ya nchi zilizo jirani.

Ugumu mmoja wa mpango huu mpya ni mtindo wa sasa wa mitihani. Kama wanafunzi wanatumia wakati mwingi zaidi wakijifunza kazi za mikono, na katika kufanya kazi zingine zitakazowasaidia kuwapatia chakula wakati wa masomo yao, hawataweza kufanya mitihani ya aina ya sasa au katika muda ule ule wa mafunzo. Lakini ni vigumu kuelewa kwa nini mtindo wa sasa wa mitihani usibadilishwe. Nchi zingine zinaanza mtindo huu wa kuchagua wanafunzi wao, ama kwa kuacha mitihani kabisa toka madarasa ya chini, ama kwa kuchanganya mitihani na njia nyingine za kupima akili. Hakuna sababu Tanzania isiunganishe mtihani unaotungwa kufuatana na mafunzo yanayotolewa, pamoja na makadirio ya mwalimu ya kazi ya mwanafunzi aliyoifanya kwa ajili ya shule na kwa ajili ya kijiji. Njia hii ingefaa zaidi kuchagua wale watakaoingia katika shule za

sekondari, vyuo vya ualimu, na vyuo vikuu n.k., kuliko njia ya sasa ya kufaulu mtihani tu. Mpango kamili wa elimu ya aina mpya utakapokuwa umefanywa, itabidi suala la uchaguzi wa watoto lichunguzwe tena.

Mpango huu mpya wa kazi katika shule zetu unahitaji mabadiliko makubwa katika utaratibu wetu. Pengine itaonekana haja vile vile ya kutazama upya jinsi ya kuugawa mwaka katika vipindi vya shule, na kubadilisha mtindo wa sasa wenye likizo ndefu ndefu. Mifugo haiwezi kuachwa peke yake kwa sehemu ya mwaka, wala shamba la shule haliwezi kutoa mazao ya kutosheleza wanafunzi ikiwa wakati wa kupanda, kuvuna, au wa kupalilia watu wote wako livu. Lakini inawezekana likizo za shule zikagawanywa ili watoto wa madarasa fulani waweze kwenda livu wakati wengine wako shule, au, katika shule za sekondari ambako madarasa yana vikosi viwili viwili, kikosi kimoja kiende livu na kingine kibaki shuleni. Utaratibu kama huo ni kazi kubwa kuupanga, lakini hakuna sababu tushindwe ikiwa kweli tumeamua kufanya hivyo.

Watu wanaweza kudhania kwamba kama watoto wanafanya kazi na kujifunza wakati ule ule, basi watajifunza kidogo madarasani na kwa hiyo hatimaye wale watakaoshika kazi za ufundi hawatakuwa na ujuzi wa kutosha. Kwa kweli haidhamiriwi kwamba matokeo yake yawe namna hiyo. Kwanza mpango wa sasa wa kuwaingiza shule watoto wakiwa na umri wa miaka mitano au sita umewafanya watoto hao wasiweze kujifunza mengi katika miaka ya mwanzo ya masomo yao. Tukibadili na kuwaingiza watoto shule wakiwa na umri wa miaka saba au minane, tutaweza kuwafunza watoto hao kwa haraka zaidi. Haielekei kwamba mtoto atajifunza kidogo, kama mafunzo yanyewe yanahusu mambo anayoyaona maishani mwake.

Hata kama fikara kama hizo zingeweza kuthibitishwa, haziwezi kuwa na nguvu kuliko haja ya mabadiliko ili elimu yetu ilingane na maisha yetu katika taifa. Kwa watu wetu walio wengi jambo la maana kwao ni kuweza kuandika vizuri katika lugha ya Kiswahili, waweze kufanya hesabu, na kujua historia kidogo, na mipango ya nchi na ya serikali yao; na wakapate maarifa ya kazi zinazowapatia riziki zao. Ni muhimu kusisitiza kwamba, katika Tanzania, watu walio wengi watapata riziki zao kwa kufanya kazi katika shamba lao wenyewe au la ushirika. Ni wachache tu watakaopata riziki zao kwa kuajiriwa, na ujira wao watautumia kwa kununulia chakula, ambacho mkulima hujilimia. Masomo kama afya, jiografia, na Kiingereza ni muhimu pia, hasa kama tunawafikiria wale watakaopenda kujisomesha zaidi wenyewe maishani mwao. Lakini jambo lililo kubwa zaidi ni kwamba vijana wetu wanaomaliza masomo ya shule za msingi hawana budi waweze kuishi katika vijiji vyao, na kuvitumikia.
Mpango huo huo wa kuwafanya wanafunzi wafanane na maisha ya taifa hauna budi kufuatwa kwa wale wanaopata elimu zaidi kuliko ya sekondari. Vijana

waliopitia katika shule za namna hiyo iliyoelezwa hawawezi kusahau wajibu wao kwa wananchi, hata kama walizidi kuendelea sana kusoma baada ya kumaliza shule. Hata katika Chuo Kikuu, Chuo cha Udaktari na shule nyingi kubwa, hakuna sababu wanafunzi waendelee kufagiliwa, kufuliwa, na kuoshewa vyombo. Wala hakuna sababu wanafunzi katika vyuo hivyo wasitakiwe kutumia sehemu za likizo zao wakifanya kazi kama mazoezi ya masomo yao kwa kukisaidia kijiji.

Kwa sasa baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu hufanya kazi katika ofisi za serikali, na wakifanya hivyo hupata mishahara kama wanayopata watumishi wengine. Ingefaa zaidi, mara mpango mpya utakapokuwa tayari, wafanye kazi katika mipango yenye faida kijijini, hata kama kazi hizo haziwezi kumpa ujira wa kutosha. Kwa mfano, kufanya uchunguzi wa historia ya kijiji, au kusaidia katika kazi ya kuhesabu watu, au kushiriki katika kuwafundisha watu wazima, kufanya kazi katika hospitali n.k., zingeweza kumpa mwanafunzi mazoezi katika mambo anayoyasomea. Kwa kazi hizo wangepokea ujira unaolingana na kima cha chini cha mshahara, na ziada yoyote ambayo angaliipata mwanafunzi ingepelekwa kwenye chuo kikuu, kusaidia kulipia gharama za mwanafunzi au hata kununulia vifaa vya michezo. Kazi hiyo ihesabiwe kama sehemu ya masomo yake, na ijumlishwe katika mtihani wake. Mwanafunzi asiyependa kazi kama hizo, au asiyezifanya vema, atagundua kwamba mambo mawili yatatokea. Kwanza, wanafunzi wenzake wanaweza wakamlaumu kwa sababu ya kutosaida kwa kuinua hali ya maisha ya shule na pili, shahada atakayoipata itakuwa ya daraja la chini.

Mwisho

Elimu inayotolewa Tanzania, kwa watoto wa Tanzania, haina budi itosheleze haja za Tanzania. Haina budi ipande mawazo ya taifa la kijamaa tunalotaka kulijenga. Haina budi ikazanie kufunzwa kwa wananchi wanaojivunia uhuru na kujitegemea kwa maendeleo yao wenyewe, na ambao wanafahamu faida na shida za kushirikiana. Elimu haina budi ihakikishe kwamba wale waliosoma wanajitambua kwamba ni sehemu ya taifa, na kwamba kwa kuwa wamepata nafasi zaidi, basi wajibu wao kwa taifa ni mkubwa zaidi.

Hili si jambo linalohusu masomo na utaratibu wa shule peke yake. Maadili hufunzwa nyumbani, shuleni na vijijini: maadili hufunzwa na mazingira mtoto anamoishi. Lakini haina maana shule zetu kukazania kufunza maadili na maarifa yaliyokuwa yanafaa zamani, au yanayowafaa raia wa nchi zingine, na kumbe elimu yenyewe inapendekeza kuendelezwa kwa hali tuliyoirithi ya kuwa na tofauti baina ya raia na raia wengine. Yafaa watoto wetu waelimishwe kuwa raia wa kesho na watumishi wa wananchi walio sawa, katika taifa tunaloliunda.